

WAEBRANIA, MLANGO WA PILI ²

 Akaja kwanza, na kusoma Maandiko, ili aweze kuyalinganisha na aweze kuona kama yalikuwa ni Kweli ama hapana. Aliichukua, ile Kweli, kwa Agano la Kale. Sasa, Paulo alikuwa ni msomi wa Agano la Kale. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Alifunzwa chini ya msomi aliye maarufu sana wa siku zake, Gamalieli, msomi maarufu sana. Na Paulo alilijua Agano la Kale. Nami nafikiri kutikiwa kwake kwa kwanza, kama nilivyosema asubuhi ya leo, wakati aliposhuhudia kifo cha Stefano. Hapana budi jambo fulani lilimgusa Paulo, kwa maana katika nyaraka zake zote aliendelea kurejea kwenye hilo, “Mimi sistahili, kwa maana nililiodhi Kanisa hata kufa. Mimi ni mdogo kabisa miongoni mwao.”

⁹⁵ Loo, bali Mungu alikuwa na wazo tofauti la jambo hilo. Yeye alikuwa ni mmoja wa watu wakuu sana wa siku hizo.

Mtazame Mtakatifu Paulo, yule mtume mashuhuri

Akiwa na joho lake jeupe sana na maridadi,
(alisema mshairi)

Loo, hapana budi kutakuwako na kupaza sauti
Sote tutakapokutana Kule.

Siku ile kuu wakati nitakapomwona akipokea taji ya mfia imani, tunzo la mfia imani!

⁹⁶ Nilisimama, nikiwa na kalamu ndogo ya zamani, hapa si muda mrefu uliopita, mahali alipoandika Nyaraka hizi. Na kisha wakamkata kichwa. Kisha wakamtupa kwenye mfereji wa uchafu, apate kuchukuliwa na mfereji huo wa uchafu. Na maskini Myahudi huyu pale, alisema, “Nina alama za Yesu Kristo mwilini mwangu. Nimepigana na hayawani huko Efeso, bali nimepiga vita vizuri. Nimemaliza mwendo. Nimeilinda Imani. Na tangu sasa, nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki atanipa Siku hiyo. Wala si mimi tu, bali wale wote wanaopenda kuonekana Kwake.” Jinsi ninavyopenda jambo hilo! Loo, ninataka kuhesabiwa pamoja na hao! Tulikuwa tukiimba wimbo mmoja:

Loo, hivi ungehesabiwa kama mmojawapo wa
kundi Lake?

Hivi ungehesabiwa kama mmojawapo wa
kundi Lake?

Uwe bila waa ndani, uwe ukikesha na kungoja
kuona lile tamasha;

Yeye yuaja tena.

⁹⁷ Ninataka kuwa mmoja wao. Sasa huyo mwandishi anaendelea, akisema:

Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo tulivyosikia tusije tukayakosa.

⁹⁸ Kama tulivyofundisha juu ya hayo, asubuhi ya leo, kifungu cha 2 kinashughulikia, “Ikiwa...”

Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika...

⁹⁹ Tunaona hao malaika kuwa nani? Manabii. “Mungu alisema zamani...” Sasa, tunapaswa kutekeleza, si wazo letu wenyewe, bali Biblia. Sasa mlango wa 1, wa mlango wa 1, kifungu cha 1.

Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi...kwa njia nyingi,

¹⁰⁰ Sasa anaendelea hapa, na kusema tena.

Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika yalikuwa imara,...

Basi malaika lina maana gani? “Mjumbe.” Kama Mungu alimtia mafuta mjumbe...Na halafu kama tukiwa tumetiwa mafuta, sisi ni wajumbe wa Mungu. Sisi ni wajumbe kwa ulimwengu, balozi wa Mbinguni, tukikiri ya kwamba sisi ni wasafiri na wageni. Sisi si wa ulimwengu huu. Bali tunatafuta Mji ujao, ambao mwenye kuujenga na kuubuni ni Mungu. Hatuweki hazina humu duniani, ambamo wezi huvunja, na nondo, kutu, na kuharibu. Kwa kuwa, hazina zetu ziko Mbinguni, ambako Yesu ameketi mkono wa kuume wa Ukuu. Loo, ni jambo lenye utukufu na la fahari jinsi gani, kujua jambo hilo.

Matumaini yetu hayajajengwa juu ya pungufu ya chochote

Zaidi ya damu ya Yesu na haki Yake;

Wakati yote yaliyo karibu na nafsi yangu yakiangamia,

Ndipo Yeye ndiye tumaini langu lote na ngome yangu.

Kwake Yesu, Mwamba wenye imara, nasimama;

Mahali pengine pote ni ardhi ididimiayo,

Mahali pengine pote ni ardhi ididimiayo,

¹⁰¹ Jinsi Eddie Pruitt alivyoandika wimbo huo, katika nyakati za mateso!

Sasa, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara,...(Wakati mjumbe wa Mungu aliponena Neno, lilisimama)...na kila tuzo lilipata ujira wa haki wa tuzo;

Tutapataje kupona sasa, ikiwa hatutamsikia Kristo, Ambaye ananena kutoka Mbinguni?

Sasa angalia.

Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? . . . (Wazia jambo hilo.) . . . ambao kwanza ulianza kulinenwa na Bwana, . . .

¹⁰² Kristo alianza kazi Yake. Yeye alifanya nini? Tunamwalia, jinsi ambavyo Yeye . . . mnyenyekevu, mpole, jinsi ambavyo hakuwa mtu mkuu anayejulikana kama mwanatheolojia. Bali alikuwa ni mnyenyekevu, mpole, mwanana. Hakuwa mhubiri mkuu. Sauti Yake haikusikika mtaani.

Bali Yohana alitoka kama simba anayenguruma. Yeye alikuwa mhubiri.

¹⁰³ Yesu alikuja, si kama simba angurumaye, bali Mungu akifanya kazi pamoja Naye, akithibitisha Neno. Mungu alikuwa pamoja na Kristo. Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Enyi wanaume wa Israeli, na ninyi mkaao Yuda . . . Yesu wa Nazareti, Mtu aliyedhihirishwa na Mungu miongoni mwenu, kwa ishara na maaajabu na miujiza, ambayo Mungu alitenda kwa mkono Wake, miongoni mwenu nyote, ambapo ninyi nyote ni mashahidi.” Angalia jinsi alivyowabana. “Mlipaswa kumjua.”

¹⁰⁴ Yesu alisema, “Enyi wanafiki.” Kasema, “Mnatoka nje na kuliangalia jua, nanyi . . . Ni jekundu tena kumetanda, nanyi mnasema, ‘Kutakuwa na dhoruba.’ Na kama ni kweupe na kuna jua, ama na kadhalika, mnasema, ‘Kutakuwa na kianga.’” Kasema, “Mnaweza kuutambua uso wa mbingu, bali ishara za zamani hizi, hamwezi kuzitambua. Kwa maana kama mngalinijua Mimi, mngaliijua na siku Yangu.”

¹⁰⁵ Loo, yale angeweza kupaazia sauti usiku wa leo. Jinsi Roho Wake anavyopiga makelele kupitia kwa wahubiri Wake, “Wakati umewadia!”

Tunatambua. Tunakuwa macho kwa mabomu ya atomiki. Tunajua ni nani atakayepachukua mahali pa Clark Gables, na ni nani atakayekwenda kufanya jambo *hili*, *lile*, ama *lingine*; ama ni nani atakayekuwa makamu wa rais. Tunavutiwa na hayo, bali hatuwezi kutambua ishara za wakati. Tuko mwisho.

¹⁰⁶ Ni kitu gani? Tunavutiwa sana, “Kipindi kinachofuata cha televisheni ni kipi? Je! Susie atafanya nini?” ama jina la mwanamke huyo ni gani. “Na Arthur Godfrey anaenda wapi? Atafanya mzaha wa aina gani tena?” Sisi, kama Wakristo, tunajaza akili zetu na upuuzi kama huo, wakati tunapaswa kuwa katika maombi mahali fulani, na kuisoma Biblia, kujua ishara za wakati tunaoishi.

¹⁰⁷ Kitu gani kinachorekebisha hayo, wakati wetu, ni mimbara midhaifu, hiyo ni kweli, ambazo hazichukulii mambo kwa uzito

na kuleta Ukweli wa Injili. Itatubidi kuja kujibu kwa jambo hilo katika siku zijazo. Haitupasi kupuuzia lolote. Na watu, kama ambavyo tuko hapa kwenye Maskani hii ya Branham, kuona ishara na maajabu, na nguvu za Kristo aliyefufuka; na kisha kujua ya kwamba tungeweka muda wetu—wetuu juu ya mambo mengine, na kupuuzia kuisikiliza Sauti ya Bwana Yesu, “Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu kama huu?”

¹⁰⁸ Kifungu cha 3, ama kifungu cha 4. Hapa ndipo tulipoishia, kwenye kifungu cha 4, asubuhi ya leo.

Mungu naye akishuhudu pamoja nao, . . . (Loo, jamani!)

Mungu . . . akishuhudu pamoja nao, . . .

Sikilizeni Neno.

. . . kwa ishara . . . ajabu na miujiza ya namna nyingi, . . .

Miujiza ya *namna nyingi* ni nini? *Namna nyingi* ni nini? *Namna nyingi* inamaanisha “mingi.” “Kwa miujiza *mingi*, Mungu alishuhudia.” Ee Mungu! Ninatumaini ya kwamba litazama ndani ya mioyo yenu. Sikilizeni.

¹⁰⁹ Mimi ni mmojawapo wa wachungaji wenu, pamoja na Ndugu Neville hapa. Ninawatakeni mshuhudie. Biblia ilisema, “Kama akiinuka mmoja miongoni mwenu, naye aseme *hivi na vile*, wala halitimii, msisikilize, kwa kuwa sijanena. Lakini kama akinena kwa Jina Langu, na asemayo yaje kutimia, basi lisikieni.” Amina. “Kwa kuwa niko pamoja na nabii huyo, ama mhubiri, yeyote yule. Kama asemayo yakitimia, basi msikieni.”

¹¹⁰ Sasa, enyi wapendwa, hebu na tumsikie Yeye, Roho Mtakatifu akinena katikati yetu, akionyesha miujiza ya namna nyingi, na ishara, na maajabu. Hebu na tusi yapuuzie kama tu mambo ya kawaida yanayotukia. Hebu na tukumbuke ya kwamba ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele; akithibitisha Neno Lake. Hatuna budi kufanya jambo hilo. Loo, nawasili mfanye hivyo. Iweni waangalifu. Acheni kila kitu kingine kiwe ni cha pili, hata makazi yako, mumeo, mkeo, watoto wako. Chochote kile, kiweke nafasi ya pili. Mweke Mungu wa kwanza. Unasema, “Ndugu Branham, ati juu ya watoto wangu?” Juu ya kitu chochote kile. Mweke Mungu awe ni wa kwanza. Acha awe wa kwanza.

¹¹¹ Eliya alitoka mlimani, siku moja. Yeye alikuwa ni malaika, mjumbe, mjumbe wa Mungu, aliyetiwa mafuta. Naye akamkuta mwanamke mjane akiokota kuni mbili. Akasema, “Nenda, ukaniokee mkate mdogo, kisha uniletee maji kidogo.”

¹¹² Ndipo akasema, “Kama nafsi yako iishivyo, nina keki tu za kutosha, ama kitonge cha kutosha cha unga wa ngano, kuoka mkate mmoja mdogo. Nami nina mafuta ya kutosha tu ya kwenda, kuuchanganyia, nipate kuuoka. Nami ninaokota kuni

mbili.” Njia ya mtindo wa kale ilikuwa, ndiyo njia ya Kihindi, ya kulingamisha kuni na kuzichoma kuanzia katikati, na kuendelea kuzisukuma ndani. Nimewasha mioto mingi ya kambi namna hiyo. Kasema, “Na ninaenda kupika mkate huo mdogo kwa ajili yangu na mvulana wangu, mtoto wangu mchanga. Nasi tunaenda kuula na tukafe.” Kulikuwa na ukame kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita, hakuna maji mahali popote.

¹¹³ Maskini nabii huyo thabiti, mzee, alimwangukia mwanamke huyo usoni. Akasema, “Nenda, kaniokee mimi keki kwanza.” Ni amri ya jinsi gani, kwa mwanamume kumwambia mwanamke mjane, anayekufa kwa njaa, ati amlishe yeye kwanza. Yeye alisema nini? “Kwa kuwa BWANA ASEMA HIVI, lile pipa halitapunguka, wala chupa haitaisha, mpaka Mungu atakapoleta mvua juu ya nchi.”

Kwanza, Mungu. Aliingia ndani na akamwokea mkate huo mdogo, kisha akaja akampa nabii. Akarudi moja kwa moja na kuoka mwingine, na mwingine, na mwingine, na mwingine. Wala lile pipa halikupunguka, wala chupa haikuisha, mpaka Mungu alipotuma mvua juu ya nchi. Yeye alimweka Mungu mbele ya watoto wake. Alimweka Mungu mbele ya kitu kingine chochote. Aliuchukua Ufalme wa Mungu, kwanza.

¹¹⁴ Mungu hana budi kuchukua nafasi ya kwanza moyoni mwako, nafasi ya kwanza maishani mwako, mahali pa kwanza katika kila kitu ufanyacho ama chochote ulicho. Mungu hana budi kuwa ni wa kwanza. Yeye hataki nafasi ya pili. Hastahili nafasi ya pili. Yeye anastahili kilicho bora sana, na cha kwanza, na yote tuliyo nayo. Anastahili. Jina Lake takatifu litukuzwe!

Mungu naye akishuhudu pamoja . . . yeye alishuhudu, alitoa ushuhuda, kwa ishara na maajabu . . . miujiza ya namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe?

¹¹⁵ Si yale watu wanayosema, yale kanisa liliyosema, bali ni yale yaliyokuwa mapenzi ya Mungu. Loo, tunahitaji kutafuta mapenzi ya Mungu, si hisani za jirani yako, si fadhili za watoto wako, si fadhili za mumeo au mke wako. Bali, tafuta mapenzi ya Mungu, na utimize hayo kwanza. Ndipo mengine yote, ridhaa ya mke na ridhaa ya watoto, zitaambatana moja kwa moja na hayo. Lakini, mweke Mungu kwanza.

¹¹⁶ Angalia, sasa.

Maana hakuuweka chini ya malaika ulimwengu ule ujao tunaounena,

¹¹⁷ Vinginevyo, wale Malaika wakuu wanaohudumia Mbinguni, Gabrieli, Mikaeli, Pakanga, na elfu kumi mara elfu kumi ya Malaika wa Mbinguni; ama makumi ya mamia ya manabii ambao wamekuwa hapa duniani, kila mmoja wao; Yeye kamwe hajaweka yeyote wao kuwa na mamlaka juu ya ulimwengu ujao, tunaounena. Si hata mmoja! Yeye hakusema kamwe, “Isaya,

utautawala ulimwengu.” Yeye hakuuweka ulimwengu kamwe chini ya utawala wa Eliya. Wala hakuuweka chini ya Gabrieli, wala malaika yeyote, roho yeyote ahudumuye.

118 Angalia yale aliyosema, Paulo, angali akimtukuza Kristo, ambaye tunamkena.

Ila mtu mmoja ameshuhudia hivi mahali fulani, akisema, Mwanadamu ni nini hata umkumbuke, ama mwana wa binadamu, hata umtembelee?

Umefanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mkono wako;

119 Sasa, ukitaka kusoma hayo, ni Zaburi 8:4-6, Daudi akinena. Sasa yeye alimwita nini Daudi hapa? Hilo linamaliza mambo yote, papo hapo, kama ilikuwa ni kweli asubuhi ya leo, juu ya nabii.

120 Alisema, “Kwa kuwa mmoja wa malaika alisema mahali fulani.” Daudi, mjumbe wa Mungu, alikuwa ni malaika wa Mungu, kwa kuwa alikuwa ni mjumbe wa Mungu. Huyu malaika alisema, Daudi alisema, katika Zaburi, “Ulimfanya mdogo punde kuliko Malaika wa Mbinguni.” Malaika alisema ya kwamba Mungu alimfanya punde mdogo kuliko Malaika, apate kumvika taji; na apate kuteseka na kuonja mauti, apate kutukuzwa tena. Apate kumfanya aninii. . . arithi vitu vyote vya ulimwenguni. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

121 Sasa, katika—katika Mathayo 28:18, tunasoma haya. Baada ya Yeye kusulibishwa na kufufuka tena katika siku ya tatu, alikutana na wanafunzi Wake na kuwaagiza waende ulimwenguni kote, wakaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Alisema, “Nimepewa mamlaka yote Mbinguni na duniani mikononi Mwangu. Mamlaka yote Mbinguni, mamlaka yote duniani, nimepewa Mimi.” Ilikuwa ni nini? Mwanadamu na Mungu walikwishaungana. Yule Logos alikuwa amefanyika mwili na kuuawa, na akafufuka tena kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu, Naye alikuwa basi Imanueli aliyetiwa mafuta milele na milele. Mungu alibadilisha makazi Yake, kutoka katika Kiti cha Enzi huko kwenye hizo anga, akakaa kwenye moyo wa Mwanawe, Kristo Yesu, apate kuishi na kutawala milele. “Mungu alikuwa ndani ya Kristo.” Yeye Ndiye mahali pa mwisho pa Roho pa kupumzikia.

122 Roho alikaa kwenye maskani, wakati mmoja, mwajua jambo hilo, chini ya hema. “Naye Sulemani alimjengea nyumba. Bali, hata hivyo Yeye, Aliye Juu haishi katika nyumba zilizojengwa kwa mikono.” “Bali mwili umeniumbia.”

123 Kwenye Kitabu cha Matendo, mlango wa 7, wakati alipokuwa akinena, yeye alisema, “Wote walitangulia kuona jambo Hilo. Walimjengea hema, Musa alimjengea, alikuwa na

hema, kisha akaweka humo sanduku la agano, kwa kuwa Mungu alikuwa kwenye Kiti cha Rehema. Hakuishi mle.” Vema.

¹²⁴ Ndipo, “Mwili umeniambia,” mwili wa Bwana Yesu Kristo, uliofanywa punde mdogo kuliko Malaika upate kuonja mauti; wala si mwingine ila yeye hasa aliye Juu kuliko wote, Kristo; Mfalme wa Amani, Mfalme wa wafalme, Bwana wa bwana, Muumba, kila nyota ulimwenguni.

¹²⁵ Ee Mungu! Yeye alifanyika punde mdogo kuliko viumbe Vyake, apate kumkomboa mwanadamu (mwanadamu asiye na makazi, bila msaada), na kuwapa makazi Mbinguni. Aliacha fahari za Mbinguni. Aliacha Jina kuu sana lililoweza kuitwa. Na wakati alipokuwa duniani, mwanadamu alimpa jina duni kuliko yote waliloweza kumpa, wakasema, “Jambo la kwanza, alikuwa mwana haramu.” Alizaliwa horini, akafungwa matambaa yaliyotolewa nyuma ya nira ya maksai. Hana mahali pa kwenda, hakuwa na makazi ya kwenda kuishi. Naye aliitwa, “Beelzebuli,” mkuu wa pepo. Alitendewa mabaya. Alitemewa mate. Alidhihakiwa. Alikataliwa, kisha akaenda kwenye mashimo yenye kina kirefu kuliko yote, na akajidhili kwa “Makahaba walio wachafu kupindukia.” Hivyo ndivyo mwanadamu alivyomtenda.

¹²⁶ Bali Mungu alimwinua juu sana hata ingemlazimu kuangalia chini apate kuona Mbingu. Mwanadamu alimpa kiti cha chini kabisa, alimpa mahali pabaya kabisa, jina la chini kabisa. Mungu alimwinua na kumpa Kiti cha juu kabisa, na Jina la juu kabisa. Hiyo ndiyo tofauti na yale mwanadamu aliyomfanyia Mwana wa Mungu, na yale Mungu aliyomfanyia Mwana wa Mungu.

¹²⁷ Aliinama, tupate kuinuliwa. Alifanyika sisi, ili sisi kwa neema Yake tupate kufanyika Yeye. Alikuwa kwa wasio na makao, naye akawa hana makao Yeye Mwenyewe, ili tupate kuwa na makao. Alikuwa kwa wagonjwa Naye Mwenyewe akafanywa mgonjwa, ili tupate kuponywa. Alimjia mwenye dhambi, “na akafanyika dhambi, Mwenyewe,” ili tupate kuokolewa.

¹²⁸ Si ajabu alitukuzwa. Si ajabu Yeye yuko jinsi alivyo usiku wa leo. Mungu amemwinua, na amepewa mamlaka yote Mbinguni na duniani.

¹²⁹ Wakati kazi yake ya duniani ilipokuwa imekwisha, hapa duniani. Alikuwa duniani, mara alipofanya hivyo, nyota ya asubuhi ikamtangaza kwamba ni Mwana wa Mungu. Alimtetemesha kila pepo aliyekabilia naye. Jina la Bwana na litukuzwe! Pepo walitetemeka na kupatwa na kiwewe, na kusihi wapate rehema, Uweponi Mwake. Naam, bwana. Kuzimu nzima ilijua kwamba Yeye alikuwa ni nani.

¹³⁰ Alitembea kwa unyenyekevu, hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake, kwenye usiku wa mvua. Wanyama wenyewe

aliowaumba, “Ndege wa angani wana viota, na mbweha wana mapango, bali Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa Chake kitakatifu.” Hakika, alikuwa hivyo.

¹³¹ Alifanyika dhambi, akawa duni na aliyekataliwa. Bali pepo walijua Yeye alikuwa ni nani. Walisihi wapate rehema. Walisema, “Mbona umekuja kututesa kabla wakati wetu haujafika.” Na wakati wahubiri walikuwa wakimwita, “Beelzebuli,” mpiga ramli; pepo walikuwa wakimwita, “Mwana wa Mungu aliye hai,” na kuomba wapate rehema.

¹³² Loo, jinsi ambavyo tungeweza tu kukoma kwa dakika moja! Wewe ni nani, hata hivyo? Hiyo kazi uliyo nayo ina maana gani? Ama nyumba hiyo ndogo tuliyo nayo ina maana gani? Gari tulilo nalo lina maana gani?

¹³³ Maskini ewe msichana mrembo, ewe maskini asiye na adabu, maskini sura hiyo uliyo nayo ina maana gani sasa? Enyi vijana wanaume wenye nywele zinazometameta, laini, mabega yaliyonyooka; mtainama siku moja, mtakapoinama kwa uzee.

¹³⁴ Lakini, Bwana asifiwe! Una nafsi iliyozaliwa mara ya pili. Utaishi milele na milele, kwa kuwa Yeye alifanyika wewe, ili kwamba wewe kwa neema Yake upate kufanyika Yeye, na Yeye akufanyie makao.

¹³⁵ Loo, sisi ambao tunafikiri ya kwamba tuna nguo za kubadilisha, na bidhaa chache za vyakula nyumbani, sisi ni kitu gani? Mungu angeweza kuondoa hilo kwa sekunde moja. Pumzi yako yenyewe anaishikilia mkononi Mwake. Na hapa miongoni mwetu kuwaponya wagonjwa, kutangaza na kushuhudia, na kutabiri, na kila mara ni jambo kamilifu. Na hata anahusika vya kutosha kumfufua tena maskini samaki mdogo aliyekufa, miongoni mwetu. Yehova akiwa karibu na sisi, Yehova ndani yetu, yule MIMI NIKO aliye mkuu na mwenye nguvu.

¹³⁶ Alipokufa, walidhani wamempata. Alishuka akaingia kuzimu. Alipoondoka duniani siku hiyo wakati aliposulibiwa, alienda katika ulimwengu wa waliopotea. Biblia ilisema, “Alienda na akazihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni, zisizotubu katika ule uvumilivu, zile siku za Nuhu.” Alipokufa, na Roho Yake ikamwacha, alifanyika Logos tena. Yeye, ninaona, alisema, “Nilitoka kwa Mungu. Ninarudi kwa Mungu.”

¹³⁷ Na Mungu alikuwa ni ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wale wana nyikani. Na wakati alipokuwa hapa duniani... Na wakati alipokufa, aligeuka tena kuwa Nuru. Paulo alimwona, Naye alikuwa ni Nuru. Hakuna hata mmoja wa hao wengine aliyemwona. Walimwona Paulo akianguka. Kitu fulani kilimshukia, Nacho kilikuwa ni Nuru. Paulo akasema, “Ni nani Huyo ninayemwudhi?”

¹³⁸ Akasema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Kasema, “Ni Nani Huyo?”

139 Akasema, “Mimi ni Yesu, ambaye unamwudhi, na ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo.”

140 Ndipo akaenda na kuichunguza hiyo Nuru. Paulo alirejea kwenye Biblia, apate kuona hiyo Nuru ilikuwa ni kitu gani. Ndipo akaandika Waraka huu. Yeye ni Yehova yeye yule. Nuru ile ile iliyokuwa nyikani pamoja na wana wa Israeli. Na wakati Petro alipokuwa gerezani, Yeye alikuwa ni Nuru iliyoingia na kuifungua milango.

141 Na kwa neema Yake, ili kwamba mtu yeyote asiwe na udhuru wowote... Loo, laiti wangaliweza kuwasahau hao wajumbe wasio na elimu, na wakumbuke: si huyo mjumbe, ni huo Ujumbe. Yeye ameshuka tena, kuwa pamoja nasi, katika umbo la Nguzo ya Moto. Naye anasogea na miujiza Yake ile ile na ishara, hakuna kitu kilicho nje ya Biblia; akidumu juu ya alama kabisa na Biblia, akiiweka wazi, akifunua utukufu Wake, akionyesha nguvu Zake. Jina Lake takatifu na litukuzwe!

142 Ninajua hapana budi mnafikiri mimi ni mwenda wazimu; lakini, loo, ile Raha ya Milele iliyobarikiwa iliyo ndani ya nafsi yangu. Ingawa dhoruba zinaweza kuvuma, nanga yangu inashikilia kwenye pazia.

143 Na kumwona Yeye wakati alipokufa, hata, mwezi ulishikwa na unyong’onyevu wa wasiwasi. Jua lilitua katikati ya mchana. Na alipoenda kwenye ulimwengu wa waliopotea, [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara nne—Mh.] alipiga hodi mlangoni, ndipo mlango ukafunguka wazi. Biblia ilisema, “Alizihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni, zisizotubu katika uvumilivu katika siku za Nuhu, baada ya yeye kuiaga dunia hii. Ndugu yangu na dada yangu, wakati Yeye alipokufa, kazi Yake ya duniani ilikuwa imekwisha, bali angali alikuwa anafanya kazi. Naye angali yuko kazini usiku wa leo. Amina.

144 Yeye alibisha kwenye milango ya waliopotea. Biblia ilisema alibisha. Naye akashuhudia, “Mimi ndiye ule Uzao wa yule mwanamke. Mimi Ndimi Yule ambaye Adamu alinena habari Zake. Mimi Ndimi Yule ambaye Henoko alisema angekuja na makumi elfu ya watakatifu Wake. Mimi ni Mwana wa Mungu aliye Hai, nanyi mlitenda dhambi mkavuka siku yenu ya neema. Lakini ilitabiriwa kwenu, na malaika, Henoko, Nuhu, ya kwamba sina budi kuja kutimiza kila Neno la Biblia ya Mungu. Mimi niko hapa kama shahidi katika ‘nchi hii ya waliopotea.’” Naye akawahubiri.

Huyoo akashuka moja kwa moja akaenda kuzimu, moja kwa moja hadi kwenye milango ya kuzimu, akapiga hodi mlangoni. Ibilisi akafungua mlango, akasema, “Sasa nimekupata.”

145 Akanyakua funguo hizo kutoka ubavuni mwake, akasema, “Wewe Ibilisi, umedanganya kwa muda mrefu.” Hili hapa, papa hapa kwenye Biblia. Nitalifikia mnamo dakika moja. “Umedanganya kwa muda mrefu, bali nimekuja kuchukua

mamlaka.” Akamnyang’anya funguo hizo na akampiga teke akamrudisha ndani, kisha akafunga mlango.

Akapita na kumchukua Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Siku ya tatu akafufuka, na hao waliolala mauti kaburini wakafufuka pamoja Naye. Loo, haleluya! Si ajabu yule mshairi alisema:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele,
Siku moja Yeye yuaja, loo, Siku yenye utukufu.

¹⁴⁶ Kibarikiwe kifungo kinachoifunga mioyo yetu kwa ushirika wa Kikristo, upendo wa Mungu. Wakati alipofufuka, hakuwa amemaliza, bado. Alikuwa na kazi zaidi ya kufanya.

¹⁴⁷ Biblia ilisema, “Alipaa Juu na akawapa wanadamu vipawa.” Kulikuwa na mazingira yaliyokuwa yakining’inia juu ya dunia, ya giza, ya utusitusi, ya mauti, na uchovu. Maombi yasingeweza kufika juu, kwa maana Upatanisho haukuwa umefanywa. Lakini, Yeye alipasua na kupita kwenye pazia hilo. Akafungua njia. Akapasua pazia la magonjwa. Akapasua pazia la dhambi. Akapasua pazia la uchovu. Akapasua pazia la wenye huzuni. Akapasua kila pazia, na akaweka njia kuu kwa ajili ya msafiri, anayetembea akienda kwenye barabara kuu ya Mfalme. Loo, jamani, wakati alipopita mwezi na nyota, akazidi kusonga mbele!

¹⁴⁸ Nyuma Yake, walifuata watakatifu wa Agano la Kale, Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Walienda moja kwa moja wakaingia mbingu za Mbinguni. Walipokuwa mbali sana na ule Mji, ninaweza kuwaona wakiinua macho yao. Ibrahimu akasema, “Ule pale ule Mji niliotamani kuuona. Loo, njoo hapa, Isaka. Njoo hapa, Yakobo. Loo, sisi tulikuwa wasafiri na wageni wa duniani, bali ule pale ule Mji. Ule Ndio ambao tumeungojea.”

¹⁴⁹ Na Biblia ilisema walisema kwa sauti kuu, “Inukeni, enyi malango ya milele, na mwinuke, kwa kuwa Mfalme wa Utukufu anaingia.”

¹⁵⁰ Ndipo Malaika waliokuwa nyuma ya hayo malango wakawajibu hawa malaika hapa nyuma kwa sauti kuu, na kusema, “Ni nani huyu Mfalme wa Utukufu?”

¹⁵¹ Ndipo hawa malaika waliokuwa hapa nje, hao manabii, wakasema, “Bwana wa Majeshi, Mwenye Nguvu katika Vita.”

¹⁵² Ndipo wakabonyeza vitufe na huo mlango mkubwa ukafunguka wazi. Huyoo moja kwa moja katikati ya mitaa Yeye akaja, yule Mshindi, akishangiliwa, akiwa na watakatifu wa Agano la Kale wakifuata nyuma Yake. Akaketi kwenye Kiti cha Enzi, kasema, “Baba, hawa hapa. Ni Wako.”

¹⁵³ Akasema, “Panda hapa na uketi chini, mpaka nitakapowafanya adui wako wote kuwa chini ya miguu Yako.” Tunaposoma, tunaona hayo hapa katika Maandiko. Vema.

154 Sikilizeni sasa. Nasi tuko kwenye kifungu cha 8.

Ndipo yeye ameweka *vitu vyote chini* ya nyayo zake.
Kwa maana . . . ameweka vitu vyote chini ya miguu yake
hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa
bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake,

Hayo ni, mauti. Hatuoni mauti, bado, kwa maana tungali tunakufa. Tunaona mauti.

Lakini, kifungu cha 9, “Lakini tunamwona Yesu!” Amina. Sikilizeni.

. . . twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko
malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti,
amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya
Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu.

Ni kwa nini alifanywa mdogo punde kuliko Malaika? Apate kuonja mauti. Ilibidi afe. Ilibidi aje, apate kufa.

155 Angalia hapa, ewe mpendwa. Usininii, kamwe usisahau jambo hili. Wakati Yesu alipokuwa akienda, akipanda kile kilima, mauti ilikuwa ikivuma karibu na kichwa Chake.

156 Hebu na tuichukue picha yetu twende mpaka huko Yerusalemu, miaka elfu mbili iliyopita. Nawe ungewezaje kuikataa? Ninasikia sauti ikija kupitia mtaani. Ni kitu gani? Ni kitu fulani kinachogongagonga. Ni msalaba wa kale unaoparuza unaoshuka, ukitoka kwenye malango ya Dameski, ukigongagonga kwenye mawe ya mango yaliyojengea barabara. Hayo mawe makubwa ya mango yangali yako kule. Ukigongagonga kwenye mawe haya makubwa ya mango, pump-pump. Ninaona matone ya Damu kwenye barabara ya mji. Ni kitu gani? Ni Mtu mmoja asiye na hatia; hajafanya lolote ila yaliyo mema. Watu walikuwa ni vipofu. Hawakumjua. Hawakumtambua.

Unasema, “Ati ni vipofu? Je! Wangeweza kuwa na macho?”

157 Inawezekana bado uwe ungali una macho na uwe ni kipofu. Unaamini jambo hilo? Biblia ilisema hivyo. Mnamkumbuka Elisha kule Dothani? Alitoka akaenda akawapiga hao watu kwa upofu, akasema, “Sasa nifuatani.” Walikuwa vipofu kwake.

158 Na watu ni vipofu usiku wa leo. Kanisa fulani lisiloamini katika uponyaji wa Kiungu, lilikuja kwangu wakati mmoja, na kusema, “Nipige upofu. Nipige upofu.” Ilikuwa ni nyumbani kwa Ndugu Wright. Kasema, “Nipige upofu.” Kasema, “Paulo alimpiga mtu mmoja kwa upofu, wakati mmoja.” Kasema, “Nipige upofu.”

159 Nikasema, “Rafiki, Ibilisi tayari amefanya jambo hilo. Wewe tayari ni kipofu. Hakika, ndivyo ulivyo.”

160 Akasema, “Mponye msichana huyu mdogo nami nitakuamini.”

161 Nikasema, “Mwokoe yule mwenye dhambi nami nitakuamini.” Hakika.

162 “Loo,” akasema, “hana budi kuamini.”

163 Nikasema, “Jambo lile lile hapa, halina budi kuja kupitia katika neema kuu ya Mungu.”

164 Ibilisi, mu—mungu wa dunia hii, ameyapofusha macho ya watu. “Wana macho lakini hawawezi kuona,” Biblia ilisema.

165 Huyu hapa, akipanda kwenda zake barabarani, akikokota alama za miguu zenye Damu akipanda barabarani. *Nyuki* wa mauti alikuwa akichoma-choma karibu Naye, akimvumia, “Ni muda kidogo tu nitakupata.” Alikuwa anadhoofika, akiona kiu ya maji.

166 Nilipigwa risasi wakati mmoja, nikiwa nimelala hapa kondeni, damu ikitiririka tu kutoka kwangu. Nilipiga makelele nipewe maji. Ndipo rafiki wangu msiri akakimbia, akachukua kofia yake akaitumbukiza majini, maji ya siku nyingi sana yaliyosimama, vifurukuta mikia vikiwa ndani ya maji hayo. Akaja, nami nikafungua kinywa changu; akaikamua hiyo. Kwa sababu, damu ilikuwa ikibubujika kama chemchemi, pale mahali ambapo nilikuwa nimevunjwawunjwa na risasi ya bunduki. Nikiona kiu!

167 Kwa hiyo ninajua kile Bwana wangu hapana budi alikuwaje, baada ya kutokwa na damu asubuhi hiyo yote, tangu saa tatu hadi saa tisa jioni, akipoteza Damu hiyo yote. Ninaona joho Lake, kwanza, likiwa kama lenye madoa madogo-madogo. Na madoa hayo yote yanaanza kuwa makubwa na kuungana, yanafanya tone moja pana na kubwa la Damu, likimdongokea mguuni alipokuwa akitembea. Hiyo ilikuwa ni Damu ya Imanueli. Loo, dunia haikuistahili.

168 Lakini wakati anapopanda juu, *nyuki* huyu akiwa anachoma pande zote. Alifanya nini? Hatimaye alimdunga mwiba.

Lakini, ndugu, mtu yeyote anajua, ya kwamba mdudu ama nyuki, kama akiwahi kukuuma mara moja, jambo hilo linamaliza kazi ya kuuma. Hawezi kuuma tena. Kwa sababu, anapoondoka, anatoa mwiba wake.

Hiyo ndiyo sababu ilibidi Mungu afanyike mwili. Aliuchukua mwiba wa mauti akautia mwilini Mwake, na akauchomoa toka kwa mauti. Jina la Bwana na litukuzwe! Mauti inaweza kuvuma na kuuma, bali haiwezi kukudhuru.

169 Paulo, wakati alipomsikia huyo *nyuki* akivuma karibu naye, mauti ilikuwa ikija moja kwa moja. Akasema, “U wapi, Ewe mauti, uchungu wako?” Aliweza kuelekeza kidole huko Kalvari mahali ambako uliachwa katika mwili wa Imanueli. “U wapi ushindi wako? Lakini Mungu ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Naam.

170 Hatuoni mambo yote.

Ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani, Yesu, kwa sababu ya maumivu ya mauti, . . .

Kwa kuwa imempasa yeye, ambaye kwa ajili yake na kwa njia yake vitu vyote—vyote vimekuwapo, ambaye kwa yeye tuna vitu vyote, hapo mwan- . . . wana wengi . . . na kufanywa kiongozi mkuu wa wokovu wetu . . . kwa njia ya mateso.

Njia pekee angaliweza kufanyika Kiongozi wa wokovu wetu, ilibidi ateseke.

¹⁷¹ Sikilizeni Maneno haya mazuri hapa sasa. Sasa sikilizeni.

Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote . . . mmoja: . . .

Loo, hivi hamwoni Mzabibu na Tawi pale? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wote ni Mmoja.

. . . kwa ajili hii haoni haya kuitwa ndugu zake,

Unaona? Kwa nini? Sikilizeni, kifungu kifuatacho.

Akisema, Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kanisa nitakuambia sifa.

Na tena, nitakuwa nimemtumaini yeye. Na tena, Tazama, mimi nipo hapa na watoto ulionipa Wewe.

Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye huyo aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi,

Awaache huru wale ambao kwa . . . kwa ninii . . . kwa . . . kwa hofu ya mauti daima waliwekwa katika hali ya utumwa.

¹⁷² Mwanadamu daima amehofu mauti. Kristo alifanyika dhambi, akafanywa duni, apate kuitwaa mauti katika nafsi Yake. Wala Yeye haoni haya kuitwa “Ndugu” yetu, kwa kuwa alijaribiwa kama vile tu tunavyojaribiwa. Naye anaweza kufanya ninii . . . awe mwombezi anayefaa, maana alistahimili jaribio la namna ile ile unalostahimili. Naye alipachukua mahali pako, akijua ya kwamba usingeweza kupachukua wewe mwenyewe.

¹⁷³ Kwa hiyo, hivi huoni, ndugu, dada? Jambo hilo lote ni neema. Yote ni neema. Si yale ufanyayo, hata hivyo. Ni yale Yeye aliyokwisha kukufanyia. Sasa, huwezi kufanya jambo hata moja kustahili wokovu wako. Wokovu wako ni karama. Kristo alifanyika dhambi, upate kuwa mwenye haki. Naye Ndiye Kiongozi Mkuu anayefaa kwa wokovu wetu, kwa maana Yeye aliteseka kama jinsi vile tu tulivyoteseka. Amejaribiwa kama vile tu tunavyojaribiwa. Wala haoni haya kuitwa “Ndugu yetu,” maana Yeye anajua yale tunayopitia. Loo, Jina Lake lihimidiwe!

Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu.

¹⁷⁴ Loo, jamani! Yeye hakufanyika Malaika. Alifanyika Uzao wa Ibrahimu. “Nasi, tukiwa wafu katika Kristo, tunakuwa Uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi kulingana na ahadi.” Unaona? Yeye hata kidogo hakuchukua asili ya Malaika. Hakuwa Malaika kamwe. Yeye alifanyika Mwanadamu. Alifanyika Mzao wa Ibrahimu, kisha akachukua mwiba wa mauti katika mwili Wake Mwenyewe, apate kutupatanisha turudi kwa Mungu, na sasa ameketi huko kama Mwombezi. Jamani, tungewezaje kukataa jambo Hilo, ewe mpendwa?

¹⁷⁵ Sikilizeni.

Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu... dhambi za watu wake.

¹⁷⁶ Apate kuwa Mpatanishi! Unaona, kulikuwako na uadui kati ya Mungu na mwanadamu. Wala hakuna mtu...

Waliwatuma malaika, manabii. Wasingeweza kupachukua mahali pako, kwa kuwa ilibidi wajiombe wenyewe. Wasingeweza kupachukua mahali hapo.

¹⁷⁷ Ndipo, Yeye akatuma sheria. Torati ilikuwa ni polisi aliyetuweka gerezani. Isingeweza kututoa. Yeye alituma sheria.

Aliwatuma manabii, aliwatuma wenye haki, na kila kitu, wasingeweza kufanya upatanisho. Bali alishuka na akafanyika mmoja wetu. Loo, jamani!

¹⁷⁸ Laiti tungalikuwa na wakati zaidi hivi sasa, ningetaka kuwapeleka kwenye ile sheria ya ukombozi; bali hatuna, lakini kwa muda kidogo tu. Picha hiyo nzuri iko kwa Ruthu na Naomi. Kama utaona pale, ule upatanisho, jinsi vile ambavyo mkulima, mtu ambaye alipaswa kukomboa shamba lililopotezwa na kuhasirika, ilibidi awe ni jamaa wa karibu wa mtu aliyepoteza shamba hilo. Hiyo ndiyo sababu ilibidi Boazi awe ninii... alikuwa ni wa jamaa ya karibu kwa Naomi, hivi kwamba aweze kumpata Ruthu. Na baadaye, ilibidi awe anastahili. Ilibidi awe na uwezo wa kufanya hivyo, apate kukomboa kilichopotea. Ndipo Boazi, hapo langoni, akatoa ushuhuda wa hadharani, kwa kuvua kiatu chake, ya kwamba alikuwa amekomboa Naomi na mali yake yote. Naye alipaswa kuwa ni jamaa wa karibu.

¹⁷⁹ Na hiyo ndiyo sababu ambayo Kristo, Mungu, ilibidi awe jamaa yetu wa karibu. Naye alishuka na akawa Mwanadamu. Naye alipitia majaribu. Na alichekwa, akadhihakiwa, na kuteswa, na kupuuzwa, na kuitwa “Beelzebuli,” na—na kumtweza, na kukubali mauti chini ya adhabu ya kifo. Unaona? Ilibidi awe jamaa yetu wa karibu. Ilibidi ashitakiwe kwa kusingiziwa, kwa kuwa wewe unasingiziwa kwa uongo. Ilibidi

astahimili magonjwa, kwa kuwa wewe ni mgonjwa. Ilibidi azichukue dhambi, kwa maana zilikuwa ni dhambi zako. Na ilibidi awe jamaa wa karibu. Njia pekee angaliweza kutukomboa ilikuwa ni kuwa jamaa yetu wa karibu. Na jinsi alivyofanyika jamaa yetu wa karibu, ni kwa kuchukua mfano wa mwili wenye dhambi na kufanyika mmoja wetu. Na katika kufanya jambo hilo, Yeye alilipa hilo deni na akatukomboa kuturudisha katika ushiriki wa Baba. Loo, ni Mwokozi jinsi gani! Maneno yasingeweza kuelezea jambo hilo.

Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa akipasiwa ninii... na kwamba aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.

¹⁸⁰ *Kuwasaidia* kunamaanisha “kuwahurumia.” Ni kwamba, sababu ya Yeye kufanyika *hivi*, ni ili kwamba apate kuwa na huruma na ninyi ambao mnaninii... mlio na *heri* zenu na *shari*, na matatizo yenu *madogomadogo*, na majaribu yenu yanakuwa makubwa sana ni vigumu kwenu kuyavumilia. Yeye anajua jinsi ya kuwahurumia. Yeye anaketi pale, kufanya upatanisho. Anaketi pale, kuwapenda. Na ingawa unakosea, Yeye hatakuacha. Bado angali atakuja kukutafuta na kubisha moyoni mwako. Hakuna mwenye kurudi nyuma humu jengoni ila yule anayejua ya kwamba Mungu hubisha moyoni mwake kila siku. Naye atafanya hivyo mradi tu wewe ni mwanadamu humu duniani, kwa kuwa amekupenda. Alikukomboa.

¹⁸¹ Washairi wamejaribu, waandishi wamejaribu, mwanadamu amejaribu kuelezea hiyo chemchemi ya “upendo,” wala haiwezi kupatikana katika misamiati ya kibinadamu. Mtu mmoja alisema:

Loo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo tajiri na msafi!

Jinsi usivyopimika na ulivyo na nguvu!

Utadumu milele,

Wimbo wa Watakatifu na Malaika

Kama tungaliweza kuijaza bahari kwa wino,
Na kama mbingu zingetengenezwa kwa karatasi;

Kila kikonyo duniani kiwe ni unyoya wa kuandikia,

Na kila mtu kazi yake iwe ni mwandishi;

Kuandika upendo wa Mungu aliye juu

Kungeikausha bahari;

Wala gombo lisingalienea yote,

Hata kama lingetandazwa kote mbinguni.

¹⁸² Kamwe hutafahamu. Hakuna njia kwetu kufahamu jinsi ambavyo hiyo dhabihu kuu, aliyoitoa, ilivyoshuka na kutupatanisha kurudi kwa Mungu. Ndipo akarudi na kusema,

“Sasa, sitawaacha yatima. Nitakuja tena na niwe pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi ukamilifu wa dahari.”

¹⁸³ Nasi tupo hapa siku ya leo, tukiishi katika wakati wa mwisho, tukiwa na Yesu yule yule, mambo yale yale, ishara zile zile, maajabu yale yale, wokovu ule ule, Roho yeye yule akifanya mambo yale yale, Injili ile ile, Neno lile lile, mifano ile ile, dhihirisho lile lile, kila kitu. Haitupasi kutojali wakovu huu mkuu, kwa kuwa itatubidi kutoa hesabu, siku moja, kwa yale tunayofanya na Mwana wa Mungu.

¹⁸⁴ Yuko mikononi mwako usiku wa leo, ewe mwenye dhambi, uliyerudi nyuma. Utafanyaje Naye? Unasema, “Vema, nitaliahirisha.” Lakini, kumbuka, usifanye hivyo. Hakuna njia, hata kidogo, kama wewe ni mwenye dhambi, ambapo unaweza kuondoka kwenye jengo hili na uwe vile vile. Huwezi kufanya hivyo.

¹⁸⁵ Pilato, usiku mmoja, alijaribu kufanya hivyo. Aliomba maji na akanawa mikononi yake. Akasema, “Sina uhusiano wowote Nalo. Ni kama tu kwamba sijapata kuliona. Sijapata kuisikia Injili. Sitaki kujihusisha kwa chochote Nalo.” Je! angeweza kuinawa aiondoe mikononi mwake? Asingeweza.

¹⁸⁶ Hatimaye, unajua kilichompata Pilato? Yeye alirukwa na akili. Na huko mbali sana Uswisi, tulikokuwa mwaka jana, tukihubiri Injili. Sasa kuna hekaya ya kale iliyosema, ya kwamba, kuna kidimbwi cha maji ambapo watu wanakuja kutoka ulimwenguni kote, kuangalia, kila mwaka, wakati wa kule kusulibiwa. Pilato, alijitumbukiza akafa, kwa kujiua, akiruka kujitumbukiza ndani ya maji haya na kujizamisha majini. Na kila mwaka, kwenye siku ile ile, maji ya bluu yanachemka kutoka katika kidimbwi hicho, kuonyesha ya kwamba Mungu aliyakataa hayo maji. Maji hayawezi kamwe kuosha Damu ya Yesu kutoka mikononi mwako au nafsini mwako. Kuna njia moja tu ya kufanya jambo hilo, hiyo ni kuikubali kama msamaha wako wa kibinafsi na upatanishwe kwa Mungu.

Na tuombe.

¹⁸⁷ Baba wa Mbinguni, tunakushukuru usiku wa leo kwa ajili ya Neno. “Kwa kuwa imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa Neno.” Tunakushukuru kwa ajili ya Yesu. Nasi tunapoiona siku hii kuu tunayoishi, jinsi ambavyo ishara na maajabu, jinsi tulivyoacha mambo haya yatupite. Mungu, yafungue macho ya watu katika maskani hii, usiku wa leo, wapate kuona na kufahamu ya kwamba tuko katika saa za mwisho. Wakati unapita upesi. Hatuna wakati mrefu zaidi tena wa kuwa hapa, na itatubidi kumwona Yesu. Na itatubidi tuhesabiwe kuwa ni wasaliti, kwa kuwa hakuna udhuru asubuhi ya leo. Wakati ulipotoa lile ono kubwa na kuu sana, la yule mtu kuja hapa, kutoka huko mbali barani,

na kumwona, bila shaka yoyote, akiinuka kutoka kwenye kiti cha magurudumu, akapokea kuona kwake. Miguu yake ikawa na nguvu, huyoo akipitia humu jengoni, akishangilia na kumsifu Mungu. Inaonyesha ya kwamba Mungu angali anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Kuona maono, kama alivyosema Yesu, “Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe. Siwezi kutenda neno.”

¹⁸⁸ Yule kipofu alimfuata, na akasema, “Uturehemu.”

¹⁸⁹ Akasema, aligusa macho yao na kusema, “Na iwe kwenu, kulingana na imani yenu.”

¹⁹⁰ Sasa, Bwana, tunamwona Yesu. Hatuoni mambo yote. Tunaona tungali tunawapeleka watakatifu wetu kaburini, na kutembea juu ya kaburi la sisi kwa sisi. Lakini tunamwona Yesu, aliyefanya ahadi. Tunamwona yupo pamoja nasi. Si Yesu aliye kaburini, si Yesu wa miaka elfu mbili iliyopita; bali ni Yesu usiku wa leo, aliye pamoja nasi. Tunamwona amedhihirishwa katika nguvu Zake zote, na ishara, na maajabu.

¹⁹¹ Mungu, jalia kwamba kamwe tusiupuuze Wokovu huu mkuu. Lakini jalia tuukumbatie, na kuukubali, na tuwe wenye kicho, na tuishi Kwa Huo mpaka siku atakayokuja Yesu kutuchukua atupeleke Nyumbani. Tujalie, Bwana. Tunaomba hayo katika Jina Lake.

¹⁹² Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, sijui kama yupo mtu humu jengoni usiku wa leo, chini ya Uwepo wa Kiungu wa Roho Mtakatifu, angesema, “Ndugu Branham, mimi nimeshawishika ya kwamba nimekosea. Nimeshawishika kwamba nimekosea. Mungu amenifunulia dhambi zangu. Nami ninajua ya kwamba ni mwenye dhambi. Nitamwinulia mkono wangu na kuomba rehema, usiku wa leo. Mungu, nirehemu. Nimekosea.” Ungeweza kufanya hivyo?

¹⁹³ Tunapongojea kwa muda kidogo tu, kama kuna mtu hapa anayetaka kufanya hivyo, kuna ubatizo utakaofanyika mnamo muda mchache tu. Na endapo wewe ni mwenye dhambi, mimi ningetubu. Unawezaje kukataa upendo kama huo usio na kifani wa Mtu aliyekufa? Mungu mtakatifu wa Mbinguni alifanyika Mtu mwenye dhambi; si kwa sababu alifanya dhambi, bali kwa sababu alikuwa na dhambi zako, na akazichukua pale hadi Kalvari. Hivi basi hutakubali msamaha huo? Hivi hutafanya hivyo usiku wa leo? Tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, mtu fulani na aseme, “Nikumbuke, Ndugu Branham. Ninamwinulia Kristo mikono yangu, na kusema, ‘Unirehemu. Mimi, mimi ni mwenye dhambi, nami ninataka kupatanishwa kwa Mungu.’” Je! ungeweza kuinua mkono wako?

Vema, kama kila mtu ni Mkristo, basi, hebu na tuombe.

¹⁹⁴ Baba, tunakushukuru usiku wa leo, ya kwamba kila mtu hapa ndani ni Mkristo, kwamba wameshuhudia vivyo hivyo kwa kuendelea kunyamaza, ya kwamba dhambi zao zote ziko

chini ya Damu. Nami ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Wabariki, Bwana. Loo, ninafuraha sana ya kwamba wamepata upatanisho kwa toleo la ile Damu, kwa kusikia Neno. Kuoshwa kwa maji, kwa Neno, Hilo linatusafisha. Linatuleta mahali palipo patukufu sana, ambapo—ambapo mwenye dhambi, akiwa na uovu wake mbaya sana, anafanywa mweupe kama theluji. Mawaa mekundu sana ya dhambi yameoshwa, nasi tu viumbe vipya katika Kristo. Jinsi tunavyokushukuru kwa hilo, Wewe, kwa ajili ya jambo hili.

Sasa ibada ya ubatizo inakuja. Nina habari ya kwamba maskini msichana huyu, usiku wa leo, atabatizwa hapa chini, katika Jina la Bwana wake.

¹⁹⁵ Ee Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba utambariki msichana huyu. Jinsi mawazo yangu yanavyorejea kwenye siku chache tu zilizopita, nilipokuwa nikija Henryville na kumwona maskini msichana huyo wa kupendeza akitembea kule mtaani. Na usiku wa leo, yeye ni mama, bibi. Amekukubali Wewe kama Mwokozi wake binafsi. Maisha yamekuwa ni magumu kwa mtoto huyu, Bwana, Ee Mungu, bali Mbingu ni ya hakika kwake. Nasi tunakushukuru kwa ajili ya jambo hilo. Tunaomba, Mungu, ya kwamba utambariki kijana mwanamke huyu sasa. Naye anapokuja kubatizwa kwa maji, naomba umjaze na Roho Mtakatifu wa Mungu. Jalia hilo, Bwana. Jalia nafsi yake isisimkwe sana, iingie hadi Mbinguni! Tujalie hayo kwa ajili ya utukufu Wako. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁹⁶ Ninataka kusoma kutoka Matendo, mlango wa pili; Petro akizungumza, kwenye Siku ya Pentekoste, ubatizo wa kwanza uliowahi kutekelezwa katika Kanisa la Kikristo. Petro, akiwakemea Mafarisayo na watu walio vipofu, kwa kutokumtambua Mwana wa Mungu; akiongea jinsi ambavyo Mungu alikuwa amemwinua, na kuthibitisha kazi Zake, katika ishara kuu na maajabu. Sikilizeni jambo hili, jinsi alivyosema. Alikuwa akimwinua Yesu.

¹⁹⁷ Kila roho ya Mkristo humwadhimisha Yesu, si kwa midomo yako tu, bali kwa maisha yako. Midomo yako inaweza kusema jambo moja, maisha yako yafanye lingine. Ukifanya hivyo, unajua ni kitu gani? Ni unafiki. Na ni afadhali niikabili Mbingu kama kafiri, kuliko kuwa mnafiki. Ningejaribu bahati yangu bora zaidi, ninaamini, Mbinguni, kama ka—kama kafiri, kuliko kuwa mnafiki. Hakika mimi. . . Kama ukishuhudia kwa ajili ya Yesu na kusema “Yeye ndiye Mwokozi,” ishi jinsi hiyo, maana watu watatarajia jambo hilo kwako. Hiyo ni kweli. Ishi jinsi Mkristo anavyopaswa kuishi. Tulipitia hayo asubuhi ya leo.

¹⁹⁸ Sasa, Bwana akipenda, kesho usiku, ama. . . Jumatano usiku, tunachukua mlango huu wa 3, ambao ni mlango wa kushangaza. Na sasa, hakikisheni mnajitahidi kuja Jumatano usiku. Ni

wangapi wanaokifurahia Kitabu hiki, cha fundisho hili la shule ya Jumapili? [Kusanyuiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, asanteni sana. Hilo ni jambo zuri.

¹⁹⁹ Sasa, ninataka kusoma sasa kutoka Matendo, mlango wa 2; kuanzia kifungu cha 32.

Yesu huyo, Mungu alimfufua, na sisi...tu mashahidi wake. (Wao walijua jambo hilo.)

Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia.

²⁰⁰ Sasa msikilize akinena habari za Daudi, mmoja wa wale malaika.

Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe kasema, BWANA alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume.

Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.

Daudi asingeweza kupanda juu; alikuwa chini ya damu iliyomwagika ya ndama, na mbuzi, na kondoo. Bali sasa angeweza kuinuka; alikuwa chini ya Damu ya Bwana Yesu. Kwa maana wanajibu tu kwa ile Damu wakati itakapoanza kutumika. Wakati Damu ya Kristo itakapoanza kutumika, wote wale waliokuwa wamekufa katika neema, walifufuka, hiyo ni kweli, na wakapaa Utukufuni.

²⁰¹ Sasa sikilizeni.

Basi nyumba yote ya Israeli na wajue... (Sikilizeni haya)...kwamba Mungu amemfanya Yesu huyu... mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo.

Vipi kuhusu hilo? Je! Yeye ni Nafsi ya tatu ya utatu, ama Yeye ndiye utatu mzima? Yeye ni utimilifu kamili wa Uungu, kwa jinsi ya mwili.

²⁰² Hakuna kitu kama Miungu watatu: Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Hilo hata halimo katika Maandiko, mahali popote. Halipo mahali popote. Hakuna mahali popote tulipoamriwa kubatiza “Katika jina la Baba, na katika jina la Mwana, na jina la Roho Mtakatifu,” hashia hakuna popote katika Maandiko. Ni kanuni ya imani ya Katoliki, wala si ya kanisa la Kiprotestanti. Nitamwuliza mtu yeyote anionyeshe Andiko moja ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa katika njia nyingine yoyote ila katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Njoo, ukanionyeshe jambo hilo, nami nitaweka ishara mgongoni mwangu, “Mnafiki, na nabii wa uongo, mwalimu wa uongo,” kisha nipitie mitaani. Hakuna kitu kama hicho. Kamwe hakuna mtu aliyewahi kubatizwa namna hiyo. Ni kanuni ya imani ya Kikatoliki, wala si fundisho la Kiprotestanti.

203 “Mathayo 28:19,” unasema, “Yesu alisema, ‘Basi enendeni ulimwenguni mwote, mkafundishe mataifa yote, mkawabatize kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.’” Hilo ni kweli.

Walakini si, “Katika jina la Baba, jina la Mwana, jina la Roho Mtakatifu.” *Jina* la Baba, *Jina* (si majina), la Baba . . .

Baba si jina. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Ni baba wangapi waliopo hapa? Inueni mikono yenu. Ni wanao wangapi waliopo hapa? Wainue mikono yao. Ni wanadamu wangapi waliopo hapa? Inueni mikono yenu. Vema. Sasa, jina lako ni nani? Si baba, mwana, wala mwanadamu.

204 Mwanamke mmoja aliniambia wakati mmoja, ambaye alikuwa ni kafiri hasa wa utatu, alisema, “Ndugu Branham, lakini Roho Mtakatifu ni jina.”

205 Nikasema, “Roho Mtakatifu si jina. Roho Mtakatifu ni vile alivyo. Ni Roho Mtakatifu.” Si jina; hivyo ndivyo alivyo. Mimi ni mwanadamu, bali jina langu si mwanadamu. Jina langu ni William Branham. Kwa hiyo, kama Yeye alisema, “Enendeni basi, mkayafundishe mataifa yote, mkawabatize katika *Jina* la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.”

206 Ndipo Petro, siku kumi baadaye, alisema, “Tubuni!” Sasa, hapa, sikilizeni jambo hili.

Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?”

Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

207 Je! Basi Petro alifanya yale Yesu aliyomwambia asifanye? Hakuwa amechanganyikiwa. Sisi ndio tuliochanganyikiwa.

208 Katika Matendo 2:38, Wayahudi walibatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, kwa kuzamishwa.

Katika Matendo, mlango wa 8, tunaona ya kwamba Filipo alishuka akaenda kuwahubiria Wasamaria, kisha akawabatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo, hao Wasamaria.

Katika Matendo 10:49, Petro aliwaamuru Mataifa wabatizwe katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

209 Paulo, Matendo 10:5, “Alipita kati ya nchi za juu za Efeso, akawakuta wanafunzi.” Walikuwa ni wanafunzi wa Kibaptisti; walikuwa, kila mmoja wao, Wabaptisti. Waliongoka chini ya mhubiri Mbaptisti kwa jina la—la, unaona, Apolo. Naye alikuwa ni mhubiri wa Kibaptisti, “Naye alikuwa akithibitisha kwa Biblia ya kwamba Yesu alikuwa Ndiye Kristo.”

Paulo akasema, “Je! mlipokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

210 Wakasema, “Hata hatujui kama kuna Roho Mtakatifu.”

²¹¹ Kasema, “Basi mlibatizwaje?”

²¹² Wakasema, “Tulikwisha batizwa na mtu yule yule aliyembatiza Yesu, pale kwenye kidimbwi cha maji. Huo ni mzuri kutosha.”

²¹³ Paulo akasema, “Huo hautafaa sasa. Itawabidi mbatizwe, mara nyingine tena.” Ndipo Paulo akawaamuru wabatizwe, mara nyingine tena, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Akaweka mikono yake juu yao, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yao. Hakika. Naam, bwana.

Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata;
Kwa njia ya maji, hiyo ndiyo Nuru siku hizi,
Mkizikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani;
Nuru ya jioni imekuja,
Ni wazi kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

²¹⁴ Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hiyo ni kweli. Wakati umewadia. Wakati umefika ambapo tunapaswa kutubu.

²¹⁵ Tuambieni, Pazeni sauti mtakapokuwa tayari, kwenye kidimbwi. Nasi tutaninii... [Ndugu mmoja anasema, “Tuko tayari.”—Mh.] Ati mko tayari? Vema, kuvuta mapazia.

²¹⁶ Sasa, Bwana awabariki sasa, wakati ndugu anapohudumu ubatizo. Je! nyote mnaweza kuona hapa? [Ndugu Orman Neville anawabatiza waaminio.—Mh.]



KITABU CHA WAEBRANIA

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org